# DAYOSISI YA KAKAMEGA
# MWONGOZO WA KARATASI YA TATU

## 1. SEHEMU YA A: MWONGOZO WA USHAIRI

a)

i. Mwenye tumaini/tamaa-kubwa hamu
ii. Mwenye bidii-alfajiri na, mapema, kutokwa na jasho
iii. Anayefurahia mandhari-anapotembea anasikiliza videge
iv. Mtulivu-kuna siri gani inayomliwaza
v. Aliyedhulumiwa-soko la dunia lamkaba koo
vi. Aliyeridhika-kuna jambo gani? (3×1=3)

b)

i. Inkisari-babuze-babu zake
ii. Kufinyanga sarufi/miundo ngeu ya kisintaksia-kubwa hamu-hamu kubwa (2×1=2)

c)

i. Taswira mnuso/harufu-rihi ya maua
ii. Taswira mguso-kumpapasa, kumbusu miguu
iii. Taswira usikivu-anasikiliza videge
iv. Taswira ya mwendo-yeye kuendelea kwa furaha (2×1=2)

d)

i. Tashhisi-umande kumbusu, miti kumpapasa, upepo kumpepea
ii. Kinaya-nafsineni inafurahi ilhali dunia inamhini
iii. Tashbihi-kama mtu aliye na kubwa hamu (2×1=2)

e)

i. Urudiaji wa maneno-kama-ubeti 1
 -furaha-ubeti 3
ii. Urudiaji wa sauti-a, a-ubeti 2,3
 -o, o-ubeti 3
iii. Urudiaji wa silabi-ma, ma, za, za, ha, ha (2×1=2)

f)

i. Toni ya uchungu-furaha ya mtu ni furaha gani katika dunia inayomhini?
ii. Toni ya kuajabia/kushangazwa na jambo-kuna jambo gani linamridhisha?
iii. Kuhuzunisha/masikitiko/kuhurumia-laiti angalijua

1×2=2
Kutaja-1
Kueleza-1

g)

i. Mtetezi wa haki/aliyezinduka anayelalamikia dhuluma ya wanyonge
ii. Mtu anayemtazama mkulima kipita (1×1=1)

h)

i. Lina beti tatu
ii. Kila ubeti una idadi tofauti ya mishororo na beti nyingine
iii. Kila mshororo una kipande kimoja
iv. Shairi halina mpangilio maalum wa vina
v. Idadi ya mizani katika mishororo inatofautiana (2×1)

i) Kila alfajiri na mapema ananipita na jembe na kotama katika njia inayoenda shambani kama waliyofanya mababu zake zamani; ninapomuona huwa anatabasamu kama mtu aliye na hamu kubwa. Anashika mpini na kutokwa jasho ili ajikimu (4×1=4)

## SEHEMU YA B: RIWAYA CHOZI LA HERI

2. "Dickson wewe jikaze. Mzee wako hayupo hapa…"

a) Mawazo ya Dick

Akiwa katika uwanja wa ndege akisubiri kukaguliwa

Anakumbuka hapo awali alipokuwa akitumiwa kuuza dawa za kulevya. Mara nyingine aliponea chupuchupu kunaswa ndipo angejiambia maneno haya (4×1=4)

b) Sauna alimpeleka kwa Buda ambaye alimlazimisha Dick kulangua dawa za kulevya na kuhatarisha maisha yake (alama 2)

c) Alikubali kulangua dawa za kulevya ili kuepuka adhabu ya mwajiri wake

Ili kukimu mahitaji yake, alilazimika kulangua dawa za kulevya

Kuuchukulia uamuzi wake wa kuingilia maovu kwamba ni hali aliyoandikiwa na mwenyezi mungu

Aliwazia matendo yake na kuamua kuacha ulanguzi wa dawa

Kujiendeleza kitaaluma-alisomea teknolojia ya mawasiliano

Alianzisha biashara ya vifaa vya mawasiliano (6×1=6)

d) .

i. Kubainisha migogoro katika riwaya-dickson kuibwa na sauna aliyemtosa katika ulaghai wa dawa za kulevya
ii. Kubainisha changamoto zinazowakumba watoto baada ya ndoa kuvunjika
iii. Kuwatambulisha wahusika k.m Dickson, Sauna, Buda
iv. Kuonyesha sifa za wahusika – Dickson, Sauna
v. Kuchimuza maudhui k.m ulanguzi wa dawa za kulevya, wizi wa watoto, elimu, mabadiliko
vi. Kuibua dhamira ya mwandishi k.m umuhimu wa elimu katika kujiendeleza
vii. Kuendeleza ploti-kuturudisha nyuma kwenye kisa cha Sauna kuwaiba Dick na mwaliko
viii. Hapa ndipo Umu na Dick walikutana baada ya kutenganishwa na Sauna

(Zozote 4×2)

3. a)

i. Tashhisi-Tumbo shinda hata haja ndogo haliendi!
   Sasa matumbo yalianza kudai haki…
ii. Takriri-vilio, vilio
iii. Taswira-(Sikivu) vilio vya watoto wenye njaa vilianza kusikika
iv. Nahau-pungia dunia mkono
v. Mbinu rejeshi/kisengere nyuma-waliokuwa wamebahatika kubeba nafaka…
vi. Tasfida-haja ndogo haliendi (6×1=6)

b)

i. Siasa/uchaguzi (1×2=2)
ii. Wanaorejelewa ni "Vijana"
   - Wanapalilia ufisadi kwa kutumiwa na wagombeaji uongozi kuwaibia kura
   - Wanasababisha uharibifu wa mali kwa kuchoma magari
   - Wanasababisha mauaji kwa kuwachomea watu kwenye magari. (uk 24)
   - Wanaendeleza wizi wa mali ya umma kwa kuiba kwenye maduka
   - Wanaendeleza matumizi mabaya ya vileo. Shamsi anadai kugeukia pombe kwa kuvunjikiwa
   - Wanapalilia utegemezi. Shamsi na yule kijana aliyevaa shati lililoandikwa Hitman wanaulaumu uongozi kwa misiba inayowapata
   - Wanaendeleza desturi kandamizi zinazowaletea madhara. Tuama anapashwa tohara
   - Wanashindwa kujidhibiti hisia na kuishia kujisababishia uzazi nje ya ndoa. Mfano Rehema
   - Wanaingilia burudani bila tahadhari na kusababisha maafa. Mfano Tindi, Lemi
   - Wanaendeleza unyanyasaji wa kimapenzi mabarobaro wanabaka Mwanaheri na Lime
   - Wanaendeleza ulanguzi wa dawa za kulevya. Awali Dick alitumiwa na Buda kusafirisha dawa

- Wanachangai kuzorota kwa maadili. Sauna anawauzia watu maji ya mito yakiwa kwenye chupa za 'mineral water'. (12×1=12)

4. **MWONGOZO WA TAMTHILIA**

a) Msemaji-Dina
Msemewa-Kiwa
Mahali-nyumbani mwa Dina
Ni baada ya Kiwa kumtembelea mamake. Mamake anasimulia hali ya ndoa ya Sara mwanzoni (4×1=4)

b) Takriri-Ndivyo...ndivyo
Mdokezo-ndivyo...
Kisengere nyuma-baada ya ile mvua ya baraka iliyowanyea, watu walianza tena kuwasema (2×1=)

c) Dina

i. Anajenga maudhui mbalimbali. Malezi, ushirikiano
ii. Anachimuza sifa za wahusika wengine kama vile Dina kuwa mlezi mwema
iii. Kielelezo cha watu wenye utu katika jamii. Anamsaidia dina kuandaa chakula wakati alikuwa mgonjwa
iv. Anaendeleza ploti. Anaturudisha kwa matukio ya awali kuhusu maisha ya Sara (4×1=4)

d)

i. Mwenye huruma-Sara anapougua, Dina anamsaidia kupika chakula
ii. Mwenye uhusiano mwema-anapoitwa na Sara amsaidie kupika bwana yake anaitikia wito
iii. Mwenye mapenzi ya dhati-anamsaidia rafiki yake kazi ya nyumbani (Zozote 2×1=al 2)

e)

i. Wanajamii wanasisitiza kuwa familia sharti iwe na mtoto wa kiume. Familia ya Yona inadharauliwa kwa kukosa mtoto wa kiume. (uk 10)
ii. Luka anawaalika wazee wenzake; Yona na Beni ili kuonja mavuno ya kwanza na kuibariki (uk 58)
iii. Bunju anashikilia utamaduni wa kutowakubali wazazi wake au wa Neema kulala nyumbani kwake (uk 24, 29)
iv. Sara anamweleza Asna kuwa siku zao msichana akisha baleghe ilikuwa hana amani. Lazima aozwe. (uk.52)
v. Mila na desturi za zamani zimewaumba wanaume kama watu wasioweza kusaidia katika kazi za jikoni. (uk. 66)
vi. Sara anaambia Yona kuwa fimbo wanarithi watoto wa kiume, si wa kike. (uk.2)
vii. Yona anaambia Sara kuwa fimbo ya mzee hurithiwa na mtoto wa kwanza (uk.20)
viii. Luka anaambia Yona na Beni kuwa zamani mila zao hazikuruhusu watoto wa kike kwenda skuli kurithi kitu (uk.60)

(8×1=alama 8)

5. a)

- Kuchelewa kupata Watoto-Sara na Yona waliitwa wagumba walipokaa muda mrefu bila kuzaa
- Jamii kuthamini mtoto wa kiume-watu waliwasema Yona na Sara kwa kukosa mtoto wa kiume
- Wanaume kuwapiga wake zao-Yona alivyompiga Sara kwa kukosa mtoto wa kiume
- Ulevi-Yona kuingilia ulevi
- Wanaume kutowajibikia majukumu yao-uk 14 Sara analalamika namna wanawake wanaachiwa kazi zote za nyumbani
- Kufutwa kazi-Yona alifutwa kazi ya ualimu kwa kuingilia ulevi
- Wazazi kukosa muda wa kubarizi na watoto wao-Neema alikuwa akifika nyumbani wakati Lemi ashalala, Bela aliishi akifanya kazi hadi wanawe wakapevuka wakawa watu wazima

- Watoto kulazimika kubeba majukumu ya kwao wakishaolewa-Neema alihitajika kusaidia mamake apate matibabu mjini, kumtumia babake pesa za dawa, kulipia elimu ya wanuna wake. kujengea wazazi wake nyumba
- Ukosefu wa fedha za kutosha-Bunju kuchukua mkopo wa benki
- Wazazi kutoelewana katika maswala ya ulezi wa watoto wao-Bunju anamtarajia Lemi kuamka mapema sana, kupata alama bora zaidi shuleni ilhali Neema ana maoni tofauti

(Zozote 8×1)

b)

- Asna anapenda maisha ya mjini ambapo anaweza kutafuta kazi akafanya ilhali Sara anaona kuwa ni maisha ya shida
- Asna anafurahia kuishi kwa servant quarter katika mtaa mzuri, Sara anaona chumba hicho kuwa kama kichuguu ama kizimba cha kuku
- Asna anaona afadhali umaskini na matatizo ya mjini kuliko kijijini ambako umaskini umekithiri zaidi, Sara anaona ni afadhali mtu awe maskini akiwa kwao kuliko ugenini
- Asna anathamini wembamba wa umbo lake ilhali Sara anamkejeli kwa kukonda sana
- Sara anamtarajia Asna kutafuta mume aolewe, Asna anadai hayuko tayari kuzungushwa kichwa na maisha ya ndoa
- Asna hakuridhika na usaidizi wa Bunju kwa familia yao, alimwona mkono birika ilhali Sara alishukuru kwa usaidizi wote ambao Bunju aliwapa
- Sara alitaka kurudi kijijini haraka baada ya matibabu ili akatazame mtama wake ilhali Asna alimtaka asubiri mjini hadi apate nafuu zaidi kisha babake ashughulikie majukumu ya nyumbani
- Asna aliamini kuwa angekataa kunyanyaswa na utamaduni na kuolewa alipobaleghe
- Sara aliamini ndoa ina raha kuwa wawili, Asna anaogopa ndoa ina mateso hasa kupigwa na mume

(6×1=6)

c)

- Utohozi-seli, wodi, shiti
- Tashbihi-amri na vitisho kama askari
- Taswira (mnuso)-hewa iliyojaa harufu ya dawa
- Nahau-vitanda vimesalimu amri
- Tashhisi-vitanda kusalimu amri,shiti zikagura
- Takriri-amri,amri

(6×1)

6. i)Fadhili za punda
   - ✓ Lilia ndiye alimshinikiza babake amruhusu kuolewa na Luka baadaye Luka akamgeuka
   - ✓ Pastor Lee Imani alipomtenga Lilia na Luka, Lilia alishindwa kujizuia, waliandikiana barua na jumbe za simu
   - ✓ Lilia alikubali kuacha kazi ya meneja wa benki ili kwenda kudhibiti fedha za kanisa
   - ✓ Luka alipoanza kumtesa Lilia hakuchukua hatua mwafaka za kumkomesha
   - ✓ Lilia alipoambiwa na Luka kuwa ahamie kijijini ili kuwa karibu na raia, alijinyamazia tu kama mke mtiifu
   - ✓ Alipata fununu kuwa Luka ana wanawake wengine, hakumkabili, alidhani ni uvumi tu
   - ✓ Lilia alipomkabili mumewe ofisini akiwa na mwanamke mwingine, Luka alimwamuru kurudi nyumbani naya akajiendea zake kwa vile hakupenda ugomvi
   - ✓ Lilia alipoamua kumripoti Luka kwa kituo cha polisi alibadili nia akarudi nyumbani kusubiri hatima yake
   - ✓ Mwanamke kiruka njia alifahamu kuwa Luka ana mke lakini alikubali kutumiwa kimapenzi na Luka
   - ✓ Lilia alikubali masharti ya mumewe ya kutotoka nje ya lango
   - ✓ Lilia anapigwa na mumewe hadi kuumizwa lakini hachukui hatua

   10×1

   ii) Kifo cha Suluhu

- ✓ Abigael mwenyewe alijitolea kuwa kupe kwa wanaume ili apate pesa ya kusaidia wanuna wake
- ✓ Abigael alifahamu kuwa Bwana Suluhu ana mke lakini aliamua kujihusisha naye kimapenzi
- ✓ Natasha alimchochea Abigael kumwekea Bwana Suluhu dawa ili ampore pesa watumie pamoja
- ✓ Abigael na Natasha walijirembesha ili kuwavutia wanaume zaidi
- ✓ Abigael alichoshwa na majivuno ya Suluhu lakini aliendelea kukubali kwenda chumbani kulala naye
- ✓ Bi Suluhu alifahamu kuwa Bwana Suluhu alimpachika mimba binti wa chuo kikuu. Pia alikuwa na hawara aliyempangia chumba mjini lakini hakumchukulia hatua yoyote
- ✓ Bi Suluhu aliyavumilia mateso ya mumewe kwa ajili ya watoto wao
- ✓ Bi Suluhu alijua siri za ufisadi wa mumewe, vile alifuja pesa za wananchi kwa kuwalipa wasichana wa vyuo vikuu baada ya kula uroda, lakini alinyamaza tu
- ✓ Bi Suluhu aliona kuwa ni heri yeye afe ili mumewe arejee nyumbani kuwatunza watoto wao
- ✓ Bi Suluhu aliachiwa mzigo wa kulea watoto lakini hakuchukua hatua

10×1=10

7.

a) Tashbihi-Maneno hayo yalikuwa kama hirizi
Utohozi-afisini
Takriri-tena, mwalimu, afisini
Kisengere nyuma-hata huo mwaka haukufikia nusu alipata tena habari mbaya
Nidaa-kwa vitendo!
Tashhisi-maneno...kuivaa ili yamwongoze
Taswira (oni)-mwalimu mkuu...kusoma-wahaka usoni mwake

6×1=6

b) Mrejelewa-"Fadhumo"

i. Ayasemayo mhusika-anasema kuwa hawezi kuwa kimada wa mzee aliyetaka aishi naye kama kimada-msimamo dhabiti
ii. Matendo ya mhusika-anaamua kuolewa kwa mume wa pili ili nduguye amalize shule na yeye pia atasoma-mwenye matumaini, bidi
iii. Wayasemayo wahusika wengine-mwalimu mkuu anasema wasichana wote wangalikuwa kama Fadhumo kwa bidii na utiifu, shule ingefanya vyema-mwenye bidii, mtiifu.
iv. Maelezo ya mwandishi-mwandishi anaeleza kuwa Fadhumo alikuwa amepata barua iliyokuwa imemwita katika shule moja kati ya zile nzuri katika kaunti yao-Ni mwerevu masomoni

2×1=2

c)

i. Elimu/Masomo
ii. Mwenye bidi-Anatia bidii shuleni mpaka kufikia kusifiwa na mwalimu mkuu
Mtiifu-bali na kuwa na bidi, Fadhumo alikuwa mwanafunzi mtiifu.
Mwenye msimamo dhabiti-alikuwa na kiu ya elimu hata baada ya kuolewa aliendelea na masomo ili kutimiza ndoto yake

2×1=2

iii. Ukosefu wa karo unachangia Fadhumo kukatiza elimu yake
Ndoa za mapema. Fadhumo anasitisha masomo yake na kuolewa ili aweze kuwaunza ndugu zake
Vifo vya wazazi. Vifo vya wazazi wake Fadhumo vimechangia yeye kuhangaika hasa katika kupata elimu
Utamaduni/taasubi ya kiume. Mjombake Fadhumo anapendelea kumsomesha kaka yake kwa sababu anaamini mvulana ndiye anastahili kusoma
Umaskini-wazazi wake Fadhumo hawana pesa za kutosha lakini wanajikaza kulipa karo na mahitaji mengine
Utovu wa nidhamu/ezembe miongoni mwa wanafunzi shuleni uk. 65 si watiifu
Baadhi ya wanafunzi kushindwa kukamilisha masomo yao shuleni/wengine kukamilisha japo kuwa kuchelewa. Fadhumo.

Baadhi ya wanafunzi kukosa kutangamana/ kukaa karibu na wazazi wao au jamaa zao na kusababisha msongo wa mawazo. Mfano Fadhumo

8×1=8

8. **MWONGOZO WA FASIHI SIMULIZI**

a) Ngano ya mazimwi-kuna matumizi mengi ya fantasia. Kijiwe kuongezeka umbo. (1×1=1)

b)

i. Kina umbo maalum, kwa mfano kina mwanzo. Hapo zamani za kale…
ii. Mandhari/mazingira yamesawiriwa kwa ufundi mkubwa
iii. Wahusika wamejengwa kwa ufundi mkubwa ili kusawiri tabia za wahusika katika jamii
iv. Lugha imetumika kwa ufundi. Kwa mfano lugha ya kitamathali. Kuna tashhisi, Uhuishi, takriri n.k (3×1=3)

c)

i. Zimwi kuweza kumeza umati wa watu pamoja na mifugo
ii. Watu na mifugo kutoka tumboni mwa zimwi wakiwa hai
iii. Kijiwe kuongezeka umbo na kuonekana kama kiwiliwili cha binadamu (2×1=2)

d)

i. Mtafiti atakuwa karibu zaidi na jamii na hupata habari za kuaminika
ii. Ni njia bora ya kukusanya habari kutoka kwa watu ambao hawajui kusoma na kuandika
iii. Mtafiti anaweza kuuliza maswali kuhusu kipera kinachowasilishwa
iv. Mtafiti anawezakunakili anayotazama au sikiliza na kuhifadhi sifa za kiimbo, toni..
v. Mtafiti hupata hisia halisi ya yanayowasilishwa kwa vile anakabiliana ana kwa ana na watendaji
vi. Hukuza utangamano kati ya mtafiti na wanajamii (4×1=4

e)

- ✓ Kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa ngano za mazimwi
- ✓ Kufunza shuleni
- ✓ Kutambua na kutuza wale wanaoendeleza utanzu huu
- ✓ Kuandaa tamasha na mashindano ya ngano za mazimwi
- ✓ Kufanya utafiti zaidi kuhusu ngano
- ✓ Kuchapisha vitabu zaidi vya ngano
- ✓ Kuwahimiza wazee kuwa na vikao na wajukuu ili kuwasimulia ngano
- ✓ Kupeperusha ngano kwenye vyombo vya habari (6×1=6)

f) Shughuli za kiuchumi
Biashara-soko kuu
Uchimbaji madini-pete ya dhahabu
Ufugaji-mifugo (mbuzi,kondoo, ng'ombe)
Ukulima/kilimo-wakulima makondeni

(2×1=2)

Shughuli za kijamii
Kupigana vita-wakatwaa silaha
Dini-sherehe za kumshukuru muumba
Malezi ya watoto-wanajamii kuwashauri watoto

(2×1=2)